Maisha Halisi ya Kiroho
Kuwa Mkristo wa Warumi 12
Sehemu ya 5 – Kuhudumu katika Upendo

Kushuhudia Jamii
Halisi
Warumi 12:9-13

Utangulizi

Kwa nini Wakristo wengi sana na waaminifu “hukwama kiroho?” Wanampenda Mungu, wanataka kukua, wameshuhudia kiwango fulani cha mageuzi ya kiroho, lakini, “wanakwama,” wamegonja ukuta wa kiroho. Mazoea mengine au mitazamo inaonekana haitabadilika kamwe. Kujaribu iwezekanavyo na “kumpa Yesu maisha yako tena” hudumu kwa muda mfupi. Je, utafanya nini unapokuwa umekwama kiroho?

Ukweli usiothibitishwa: Mbegu nzuri zaidi katika udongo mzuri zaidi, haiwezi kumea katika mazingira yasiyokuwa sahihi.

- **AMRI** ya Yesu inahitaji mfumo maalumu wa kiroho.

  Yohana 13:34-35

- **MFANO** wa huduma ya Yesu ya kuwakuza wanafunzi wake ilihitaji mfumo maalum wa kiikolojia

  Marko 3:13-14

- **MATENDO** ya kanisa la kwanza na mvuto wake unaunga mkono kuwepo kwa mfumo maalum wa kiikolojia.

  Matendo 2:42-47

- **HISTORIA** ya Kanisa, ya kale na ya sasa, inathibitisha mfumo maalum wa kiikolojia kwa ukuaji wa kiroho na kugeuzwa.

Hakimiliki © 2023 na Chip Ingram na Living in the Edge

Mfumo wa Kiikolojia wa Kiroho: JAMII HALISI.

Muundo ambao mfumo huu huchukua ni: KUNDI DOGO.

Tofauti muhimu: JAMII HALISI ≠ KUNDI DOGO.

Kanuni: Lazima tuhusike katika mfumo wa kiikolojia wa kiroho wa jamii halisi ili ukomavu wa kiroho uweze kutokea.

Maswali mawili muhimu:

1. Je, jamii halisi ni nini?

2. Unaweza kuipataje?

Jamii halisi hutokea wakati… **Warumi 12:9-13**

Wewe halisi… kifungu 9

…unapokutana na mahitaji halisi… kifungu 10

…kwa sababu zifaazo… kifungu 11

…katika njia sahihi. kifungu 12-13

Wewe *halisi* – Si **MFANO** wa wewe mwenyewe. Warumi 12:9

- **Uhalisia** – "*Pendo na lisiwe na unafiki .*"

- **Usafi** – "*Lichukieni lililo ovu. mkilishika lililo jema.*

Hukutana na mahitaji *halisi* – Si ya **BANDIA**. Warumi 12:10

- **Kujitoa** –*Kwa pendo la udugu, mpendane ninyi kwa ninyi."*

- **Unyenyekevu** – *"kwa heshima mkiwatanguliza wenzenu."*

Kwa sababu *sahihi* – si kwa **KUWAPENDEZA** watu. Warumi 12:11

- **Nia** – *"kwa bidii, bila kulegea; mkiwa na juhudi katika roho zenu; mkimtumikia Bwana."*
- **Njia** – "Huduma ya kweli kwa Mungu ina sifa zifuatazo:
  - Bidii – ubora
  - Msisimko – ari

Katika njia *sahihi* – Si kwa **NGUVU** zetu wenyewe. Warumi 12:12-13

- **Kuangazia Juu** – "*mkifurahi; katika dhiki, mkisubiri; mkidumu katika kusali."*

- **Kuangazia Nje** – *"kwa mahitaji ya watakatifu, mkifuata ukarimu; katika kukaribisha wageni mkijitahidi."*

Hakimiliki © 2023 na Chip Ingram na Living in the Edge

Kwa nini jamii halisi ni muhimu sana kwa Yesu?

20 "Wala si hao tu ninaowaombea; akini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. 21 Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma.

Yohana 17:20-21

Maswali ya Matumizi/Majadiliano:

1. Hebu simulia jinsi wakati fulani ulivyoshuhudia jamii halisi kwa njia muhimu na akina kaka na dada katika Kristo. (Nini kiliufanya wakati huo kuwa maalum kwako?)

2. Hebu eleza jinsi unafiki wa Mkristo ulivyokuwa kikwazo kwako.

3. Kwa nini unaona uhalisia ni muhimu sana katika mahusiano? Katika kuyagusa maisha ya watu kwa njia nzuri?

4. Je, kuna tofauti gani kati ya "mahitaji halisi" na mahitaji bandia? Je, mtazamo una jukumu gani katika kukimu mahitaji "halisi"?

5. Je, ni hatua ipi maalum ya imani/utiifu unahitaji kuichukua ili kujenga jamii halisi kwa ajili yako au mtu mwingine ili iwe jibu kwa ombi la Yesu katika Yohana 17?

Rasilimali kutoka Living on the Edge za Kukusaidia Kutumia Warumi 12:9-13

Love One Another – (Mfululizo wa CD) – Chip Ingram
Five Lies That Ruin Relationships – (Mfululizo wa CD/DVD) – Chip Ingram
Small Group Bible Studies – Yanapatikana mtandaoni kwenye LivingontheEdge.org

Hakimiliki © 2023 na Chip Ingram na Living in the Edge